


Makaratsi haya yana maelezo kuhusu Ashanti Team kinachosaidia watu wanaotoka Afrika na visiwa vya Karibe ambao wana matatizo ya akili. Kama unataka kusoma makaratsi haya kwa lugha ya Kiswahili, au kwa maandishi makubwa, au kwa maandishi ya vipofu (Braille) au kwenye kanda tafadhali piga nambari hii ya simu 01582 547659

Ashanti Community Support Team



*kusaidia watu wanaotoka
Afrika na visiwa vya Karibe
ambao wana matatizo
ya akili*

Sisi ni nani?

Kitengo cha Ashanti Team kinashirikiana na watu wanaotoka Afrika na visiwa vya Karibe ambao wana matatizo ya akili.

Tunatoa huduma yetu na kuhakikisha wateja wetu wanapata msaada wa jumuiya ili waweze kuwa na afya nzuri ya akili na wawe na uwezo wa kujitegemea.

Huduma zetu ni

- Kuwasaidia ili wakuze mtandao wa misaada katika jumuiya wanazoishi
- Kuwasaidia kutumia huduma za utimamu wa akili
- Kuwafahamisha watu wengine kuhusu mila za watu wanaotoka Afrika na visiwa vya Karibe.

Huduma

Huduma zetu ni

- Kuwasaidia na kuwashauri watu wanaoenda hospitali
- Kuwasaidia na utaratibu wa ruzuku
- Kuwaonyesha mbinu za kujitegemea
- Kuwapa ushauri
- Kusimamia vilabu ya vyakula vya Kikaribe
- Kuwasaidia na matatizo ya nyumba
- Kuwasaidia waangalizi wao

Jinsi ya kupata msaada

Daktari, mfanyakazi wa jamii, waangalizi, marafiki au ndugu zako wanaweza kuwasiliana nasi kwa niaba yako. Pia unaweza ukatupigia simu mwenyewe. Wafanyakazi wetu wanaweza kuongea Kipatois.

Tutafanya mpango wa kukutana na wewe ili tujue zaidi hali yako. Tutapanga utaratibu mzuri wa kukupa msaada unaokufaa na njia nzuri za kuzipokea. Kama kikundi cha Ashanti, ni mojawapo ya vikundi vinavyokusaidia, Mfanyakazi wa Jamii atashirikiana na wewe. Msaada utakaopokea utakuwa unaangaliwa mara kwa mara.

Huduma bora

Tunataka kuwapa wateja wetu huduma nzuri, kufuatana na sheria za halmashauri za Luton Borough Council, utaratibu na muongozo mzuri wa kazi.

Kama hujaridhika na huduma yetu, tunakushauri uonge na Mfanyakazi wako wa Jamii au na Mkurugenzi wa Kitengo. Tutasikiliza malalamiko yako na kuyashughulikia. Pia unaweza ukafuatilia Taratibu za Malalamiko za Social Services.

Namna ya kuwasiliana nasi

Saa za Kazi Jumatatu – Alhamisi 9.00am – 5.15pm

 Ijumaa 9.00am – 4.30pm



01582 560895/560852/560892

Fax

01582 490061

e-mail

AshantiHouse@luton.gov.uk

unaweza kutizama website yetu ya Council: www.luton.gov.uk